# Haki zako ukiwa kwenye kituo cha polisi

MWONGOZO UNAOHUSU WATOTO NA VIJANA

**Kijitabu hiki kinakupa taarifa muhimu kuhusu haki zako unapopelekwa katika kituo cha polisi.** Haki ni uhuru na ulinzi tulio nao sote na zinalindwa kisheria. Haki za watoto walio chini ya miaka 18 ni tofauti na za watu wazima, kwa hivyo kijitabu hiki kinaelezea kuhusu haki zako.

**Kufahamu na kuelewa haki zako kunaweza kukusaidia kujua unapotendewa haki.** Polisi wana wajibu wa kukulinda dhidi ya madhara na kutunza maslahi yako ukiwa kituoni, hata ikiwa wana ushahidi unaothibitisha kuwa umevunja sheria.


**Tafadhali soma kijitabu hiki ukipata nafasi.** Kitakusaidia kufanya maamuzi ukiwa kwenye kituo cha polisi. Atakayekupa kijitabu hiki atakusaidia kukisoma na kukielewa. Pia atakuuliza ikiwa ungependa toleo tofauti la kijitabu hiki kama vile la lugha tofauti au ambalo ni rahisi kusoma.

Children and Young People's Centre for Justice
STARR
Safer Scotland
Scottish Government

1. **Una haki ya kuelezwa sababu ya kuzuiliwa kwako kwenye kituo cha polisi.**

2. **Una haki ya kujua kwa nini polisi wamekukamata na kukupeleka kituoni.**






3. Unapaswa kuwaeleza polisi jina lako, anwani yako, tarehe ya kuzaliwa na utaifa, ikiwa unafahamu. Haya pekee ndiyo maswali unayopaswa kujibu. **Una haki ya kutojibu maswali mengine yoyote.**

4. **Una haki ya mtu mwingine kujulishwa kuwa upo kwenye kituo cha polisi.** Polisi watakuuliza ikiwa ungependa kumjulisha mtu yeyote kwamba umefikishwa kituoni. Mtu huyo anaweza kuwa mwanafamilia, mpenzi, mtunzaji, rafiki yako au mtu mnayefahamiana. Huenda usiruhusiwe kuzungumza na mtu huyu. Ikiwa hujafikisha miaka 16 au uko chini ya usimamizi, una haki ya kuandamana na mtu mwingine kwenye kituo cha polisi. Una haki ya kutembelewa na mzazi au mlezi kwenye kituo cha polisi.

5. **Una haki ya wakili kujulishwa kuwa umekamatwa na uko kwenye kituo cha polisi.** Polisi watakuuliza ikiwa ungependa kumjulisha wakili kuwa umekamatwa. Anaweza kuwa wakili wako au wakili utakayeletewa unaweza kutafutiwa wakili mwingine. Huduma hii hailipishwi.



6. **Una haki ya kuzungumza na wakili faraghani wakati wowote.** Huduma hii hailipishwi.

7. **Una haki ya kuletewa wakili unapohojiwa na polisi.** Huduma hii hailipishwi.

8. **Ikiwa hujafikisha miaka 16, sharti wakili awepo unapohojiwa na polisi, isipokuwa iwe mtu fulani yuko hatarini.** Ikiwa una miaka 16 au 17 na uko chini ya usimamizi, wakili wako sharti awepo polisi wanapokuhoji, isipokuwa katika hali zisizo za kawaida.

9. **Una haki ya kupata matibabu ikiwa wewe ni mgonjwa au umejeruhiwa. Hii inajumuisha matibabu ya afya ya kiakili.** Polisi watakuuliza maswali kuhusu afya na siha yako ili kuhakikisha unashughulikiwa inavyostahili ukiwa kituoni. Ni muhimu uwajulishe polisi ikiwa una matatizo ya kiafya ambayo huenda yakakudhuru ukiwa kwenye kituo cha polisi. Polisi wanaweza kumwomba muuguzi au daktari akuhudumie. Hii itahakikisha kuwa unatunzwa ipasavyo ukiwa kituoni. Polisi wanapaswa kukuuliza ikiwa unahitaji kuzungumza na daktari, muuguzi, au mtaalamu mwingine wa afya.

10. **Una haki ya kupewa maji na chakula.** Utapewa maji. Utapewa chakula ukikaa kituoni kwa zaidi ya saa nne. Polisi wanapaswa kukuuliza ikiwa una mahitaji maalum ya lishe kabla ya kukupa chakula.

CYCJ Children and Young People's Centre for Justice

STARR

Safer Scotland Scottish Government

# Mwongozo zaidi...

**Ikiwa unahitaji usaidizi**
Huenda ukahitaji usaidizi ili kuelewa kinachoendelea ukiwa katika kituo cha polisi. iwapo umefikisha miaka 16, usaidizi huu hutolewa na msaidizi maalum anayejulikana kama Mtu Mzima Atakayekusaidia. Huenda ukahitaji usaidizi huu ikiwa una udhaifu fulani au matatizo ya kiakili. Ikiwa polisi wanaamini kuwa unahitaji usaidizi wa Mtu Mzima Atakayekusaidia, watamleta, hata usipoulizia.

**Kupata mkalimani wa kukusaidia**
Ni muhimu kuelewa kinachosemwa katika kituo cha polisi. Ikiwa huzungumzi au huelewi Kiingereza, polisi watamleta mtu anayezungumza lugha yako ili kukusaidia. Mtu huyu anaitwa mkalimani. Huduma hii hailipishwi.

**Kupata usaidizi wa mawasiliano**
Watu wengi hutatizika kuelewa kinachoendelea katika kituo cha polisi. Polisi wanastahili kukuuliza ikiwa unahitaji usaidizi wowote au huna uhakika kuhusu kitu fulani. Wanapaswa kukupa usaidizi wa kusoma ukihitaji. Ikiwa una matatizo ya kusikia au kuzungumza, polisi watamleta mtu wa kukusaidia Mtu huyu anaweza kuwa mtafsiri wa lugha ya ishara au mtaalamu mwingine. Huduma hii hailipishwi.

**Ikiwa wewe si Mwingereza**
Iwapo wewe si raia wa Uingereza, polisi wanapaswa kuwasiliana na Ubalozi au ofisi za nchi yako, ili kuwajulisha ulipo na sababu ya kukamatwa kwako. Afisa anaweza kukutembelea kwa faragha na kupanga wakili akuone.

**Je, hatua gani itachukuliwa ukishtakiwa au ukipelekwa kituoni kufuatia agizo la kukamatwa?**
Ukishtakiwa kwa kosa, unaweza kuruhusiwa kuondoka au unaweza kusalia korokoroni kisha ufike mahakamani siku inayofuata. Iwapo umefikishwa kituoni kufuatia agizo la kukamatwa, utalala kwenye seli kisha ufikishwe mahakamani siku inayofuata. Wakati mwingine, unaweza kuruhusiwa uende nyumbani.

**Je, unaweza kuwekwa kwenye kituo cha polisi kwa muda gani?**
Polisi wanaweza kukuweka kituoni kwa hadi saa 12 bila kukushtaki kwa kosa lolote. Polisi wanaweza kuongeza muda huu hadi saa 24, ikiidhinishwa na afisa wa cheo cha juu. Una haki ya kusikilizwa kuhusu uamuzi huu, au unaweza kumpa wakili nafasi azungumze na polisi kwa niaba yako.

**Kuona stakabadhi**
Kesi yako ikipelekwa mahakamani, wewe au wakili wako atapewa stakabadhi inayoonyesha ushahidi. Hii itakuwezesha wewe au wakili wako kupanga jinsi ya kujitetea. Una haki ya kutafsiriwa maelezo haya yote, au sehemu muhimu za stakabadhi husika ikiwa huelewi Kiingereza.

CYCJ
Children and Young People's Centre for Justice
STARR
Safer Scotland
Scottish Government

# Mwongozo zaidi...

**Kuhusu haki ya kuletewa wakili**

- Polisi watakuuliza ikiwa ungependa kuzungumza na wakili. Polisi watawasiliana na wakili haraka iwezekanavyo.
- Unaruhusiwa kuzungumza na wakili wako faraghani wakati wowote. Unaweza kufanya hivyo kwa njia ya simu, au anaweza kuja kukuona kwenye kituo cha polisi.
- Kuzungumza na wakili ni jambo la kawaida, na haithibitishi kuwa umefanya kosa.
- Jukumu la wakili ni kulinda haki zako na kukushauri kuhusu sheria.
- Unaweza kuchagua kuzungumza na wakili unayemjua au wakili atakayeletwa na polisi – wakili huyu anajulikana kama wakili huru. Wakili utakayeletewa ni huru na hafanyi kazi chini ya polisi.
- Utakapohojiwa na polisi, watakuuliza ikiwa ungependa wakili awepo.
- Polisi hawaruhusiwi kukuhoji bila wakili wako kuwepo ikiwa ungependa hivyo.
- Unaweza kubadili mawazo kuhusu kuzungumza na wakili na unaweza kuomba aje wakati wowote. Wajulishe polisi haraka iwezekanavyo na watawasiliana na wakili.
- Wakili asipofika kwenye kituo cha polisi kama mlivyoelewana, au ikiwa unahitaji kuzungumza naye tena, unaweza kuwaomba polisi wawasiliane naye tena. Polisi hawahusiki na kufika kwa wakili kituoni baada ya kuwasiliana naye. Ukihitaji, polisi wanaweza kumweleza wakili kuhusu unachotaka.

**Haki ya kuwasilisha malalamishi**

- Una haki ya kuwasilisha malalamishi kuhusu jinsi ulivyotendewa na polisi.
- Kuwasilisha malalamishi dhidi ya Polisi wa Uskoti hakutakuathiri kwa njia yoyote ile.
- Unaweza kuwasilisha malalamiko ukiwa korokoroni.
- Ikiwa ungependa kuwasilisha malalamishi ukiwa korokoroni, omba uzungumze na inspekta au afisa wa cheo cha juu.
- Iwapo ungependa kuwasilisha malalamiko baada ya kuachiliwa, unaweza kwenda kituo chochote cha polisi.
- Ikiwa umeumizwa au kujeruhiwa na afisa wa polisi wakati wa kukamatwa au ukiwa kwenye kituo cha polisi, unapaswa kuwasilisha malalamiko kwa Idara ya Viwango vya Kitaalamu ya Polisi wa Uskoti.
- Ili kuwasilisha malalamiko, piga simu kwa 101 au nenda kwenye kituo cha polisi kilicho karibu nawe.
- Unaweza pia kumwomba mtu mwingine awasilishe malalamiko kwa niaba yako. Inaweza kuwa mzazi, rafiki, mwenzako au mtu unayemwamini. Unahitaji kutoa idhini yako kwa kuandika.

Kijitabu hiki kimetayarishwa na wanachama wa STARR, asasi ya kipekee inayoshughulikia maslahi ya watu nchini Uskoti, kwa ushirikiano na Kituo cha Haki kwa Watoto na Vijana (CYCJ) na Serikali ya Uskoti. ‘Haki yako ya kuwasilisha malalmishi’ imetokana na People First Scotland.

Ili upate usaidizi na maelezo zaidi, tembelea **justtherightspace.org**

© Crown copyright 2023